

Kwa Wanafamilia wa Cajon Valley,

Ninawakosa wote sana! Hii ndio mada inasikika kila mahali...”Ninawakosa wanafunzi wangu”, ”Ninawakosa walimu wangu”, ”Ninawakosa marafiki zangu”... na sisi tunawakaosa nyie wote pia! Hadi sasai tumemaliza wiki ya pili toka shule kufungwa, na ninawaandikia ili kuwapa kidogo maelezo zaidi.

Wote tunatambua kuwa hali hii imevuruga maisha yetu, na kuwa na wanafunzi nyumbani bila kutarajia inaweza kuwa ngumu kwa familia nyingi. Walimu na wafanyakazi wa shule wamekuwa wakijaribu kuwasiliana na kuangalia watoto wenu wanaendeleaje, na pia waliojitolea kusaidia kugawa chakula chetu kitamu cha asubuhi na mchana shuleni. Wilaya yetu itaendelea kutoa chakula wakati wote wa likizo ya shule isipokuwa tarehe 10/04/2020 kwa kuwa ni sikukuu.

Gavana wetu bado hajaamrisha shule za California ziendeele kufungwa mpaka mwisho mwaka wa shule, lakini tarajia uwezekano wa amri hii kutolewa, wafanyakazi wetu wanajitayarisha kutoa mafunzo ya mbali mtandaoni. Cajon Valley inakusudia kutumia mafunzo ya mbali mpaka itakapokuwa salama kwa wanafunzi na wafanyakazi kurudi shuleni.

Our Governor has not yet ordered schools in California to stay closed through the end of the school year, but anticipating the possibility of this order being made, our staff is preparing to provide online Distance Learning. Cajon Valley intends to use distance learning until it is safe for our students and staff to return to schools.

Wiki ya tarehe 23 mwezi wa 3:	Nyenzo za wanafunzi kujifunzia mtandaoni zinapatikana @ www.cajonvalley.net Machapisho ya ziada ya wanafunzi kwa ajili ya mapumziko ya Spring yatengenezwa
Wiki ya tarehe 30 mwezi wa 3:	Machapisho ya ziada yatagawiwa shuleni. Mpango wa kustawisha weledi/Kujipanga kwa ajili mafunzo ya mbali
Tarehe 6 -17 mwezi wa 4:	CVUSD Spring Break - Optional Paid Professional Learning Available Lunch Distribution Continues with volunteer support
Wiki ya tarehe 20 Mwezi wa 4:	Tunarudi shule au turadi kwenye mafunzo ya mbali mtandaoni.

Wilaya yetu imepata bahati kuwa na uwiano wa 1:1 wa chromebook na vifaa vya digital na wanafunzi wetu kutoka darasa la K - 8 hutumia kwa miaka sita sasa. Mpango wetu wa mafunzo ambao tulianza 2014 uliundwa ili kuruhusu mudazaidi kwa ajili ya walimu na wanafunzi kukutana ana kwa ana au kwenye makundi madogo. Tunapendelea msemu “ Tech kidogo...utu zaidi”. Tunavyo vifaa vya kushangaza na mtaala wa kisasa ambao uwanatayarisha watoto wetu kuwa na furaha, mahusiano mazuri na ajira nzuri, lakini siri ya haya yote iliwa na itaendelea kuwa ni walimu. Kuwaangalia, kuungana na wanafunzi wetu na kukuza mahusiano na wanafunzi wetu itaendelea kuwa lengo kuu ya kazi yetu.

Mafunzo ya mbali yatakuwa pamoja na orodha ya ujuzi wa kawaida, somo na mtaala wa kisasa wa Cajon Valley (TED Ed, World of Work, Computer Science, and Social-Emotional Learning). Tutaweza kufuatilia ushiririki na maendeleo ya mwanafunzi kwa kutumia zana za komputa, wakati tunazingatia mahitaji ya kupumzika, kucheza, kufanya mazoezi na muda wa wanafamilia wa jumuiya yetu.

Ili kuongeza fursa za kujifunza kwa wanafunzi wetu wenye ulemavu, kila mwanafunzi mwenye kipengeke 504 na/au Msimamizi wa elimu maalum atakuwa anaisaidia wilaya katika njia ya mafunzo ya mbali na kuwafikia wazazi moja kwa moja kujadili huduma zilizopo. Huduma za ziada zinaweza kuwa, lakini hazikomi hapo tu, ushauri kutoka kwa mtaalamu wa taaluma ya wanafunzi kurekebisha na/au kubadilisha mtaala kutokana na mahitaji ya mwanafunzi mwenyewe na wakishauriana na watowaji huduma wanaohusika. Kwa mfano, Huduma husika zinaweza kutolewa kupitia njia za huduma mbadala ikiwezekana huku tukizingatia kukaliana mbali kama inavyotakiwa, kuthibitisha msimamo wa wilaya wa kuwaweka wanafunzi, walimu na watoa huduma wote salama na wenye afya. Maelezo zaidi kuhusu huduma za nyongeza kwa wanafunzi wenye ulemavu zitakuja hivi karibuni

Ingawa tunategemea wanafunzi wasome kila siku na wajaribu kumaliza orodha ya masomo yao, tunataka pia walimu na wanafunzi wetu mpumzike, mkae na ndugu zenu, mfanye mazoezi na mpate hewa safi huku mkiwa mnazingatia kukaaliana mbali kwenye jamii kama ilivyopendekezwa na serikali kuu, serikari ndogo na pamoja na maafisa wa serikali.

Walimu watawasiliana na kila mmoja wenu ili kuamua ni nini itafanya kazi vizuri kwa kila familia. Tunasisitiza uwepo wa uwezo wa kubadilika ili tuweze kumudu dhiki na changamoto tupatazo wakati huu.

Tunataka kila mmoja afurahiye mapumziko wakati wa likizo(6 -17 mwezi wa 4), kwa hiyo kutakuwa hakuna mazoezi au mambo yanayohusiana na shule wakati wa kipindi hiki. Pakiti ya hiari ya kusoma na hesabu zinapatikana kwa familia wanaozitaka.

Asanteni kwa kuwaunga mkono wanafunzi wetu na nyie wenyewe. Kama watu wazima, Tunafanya kila tuwezavyo kutengeneza mazingira yaliyo salama, yenye mapenzi kwa ajili watoto wadogo kwenye maish yetu, Nawatumieni wote baraka ya afya njema! Mbaki na Nguvu! Tutayamudu haya!

Kwa Dhati,

Dr. David Miyashiro, Superintendent